

HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 22/10/2021

MAHURUDHURIO

1. HERBET BILIA - MWENYEKITI
2. TUPE KAYINGA - MJUMBE
3. GERARD MWAMHAMILA - MJUMBE
4. MWATUMU DOSSI - MJUMBE
5. DR. STEVEN NGWALE - MJUMBE

SECRETARIETI

- 1) ZABDIEL MOSHI - KATIBU
- 2) ASHA MILASI - PMU
- 3) SHURANI MPWAGE - PMU

AGENDA: BZ/2021/2022/13 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:15 asubuhi kwa kuwaeleza wajumbe kuwa kikao hicho ni maalum kwa ajili ya kujadili na kuidhinisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha aliwasihi wajumbe kuchangia kwa uhuru mada hiyo iliyokuwa mbele yao.

AGENDA: BZ/2021/2022/14 MAOMBI YA IDHINI YA KUTEKELEZA MIRADI YA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO 19 KWA UTARATIBU WA FORCE ACCOUNT.

Katibu alikielleza kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa imepokea fedha kiasi cha Tshs 660,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Uviko 19. Alieleza kuwa fedha hizo zina kusudiwa kutumika kutekeleza ujenzi wa madarasa 33 katika shule za secondary za serikali ambapo kila darasa limetengewa Tshs. 20,000,000/=

Alieleza Zaidi kuwa tayari mamlaka ya ununuzi wa Umma (PPRA) imekwishatoa mwongozo wa matumizi ya fedha hizo ambapo mojawapo ya njia za manunuzi zinazopendekezwa ni force Account chini ya kanuni ya 167 ya kanuni za manunuzi ya Umma kama ifuatavyo:-

NA.	JINA LA SHULE	IDADI MADARASA	YA	KIASI FEDHA	CHA
1	MAWELEWELE SEKONDARI	3		60,000,000/=	
2	NDULI SEKONDARI	2		40,000,000/=	
3	MKWAWA SEKONDARI	1		20,000,000/=	
4	KIGUNGAWA SEKONDARI	2		40,000,000/=	
5	MLANDEGE SEKONDARI	2		40,000,000/=	
6	KWAKILOSA SEKONDARI	1		20,000,000/=	
7	LUGALO SEKONDARI	2		40,000,000/=	
8	IPOGOLO SEKONDARI	3		60,000,000/=	

9	MTWIVILA SEKONDARI	1	20,000,000/=
10	IRINGA SEKONDARI	1	20,000,000/=
11	TAGAMENDA SEKONDARI	1	20,000,000/=
12	KRELUU SEKONDARI	3	60,000,000/=
13	MIYOMBONI SEKONDARI	1	20,000,000/=
14	KIHESA SEKONDARI	2	40,000,000/=
15	MIVINJENI SEKONDARI	1	20,000,000/=
16	MLAMKE SEKONDARI	1	20,000,000/=

Wajumbe walipokea pendekezo hilo na kulijadili ambapo mjumbe mmoja alitaka kujua iwapo kiasi hicho cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ujezi wa darasa moja cha Tshs. 20,000,000/= iwapo kitatosha. Katibu alieleza kuwa kiasi hicho ndicho kilichotolewa na serikali na ndio maana utaratibu wa force account unapendekezwa kwa lengo la kupunguza gharama. Baada ya maelezo hayo wajumbe kwa kauli moja walilidhia ujenzi wa madarasa 33 kwa gharama ya Tshs. 660,000,000/= ufanyike kwa utaratibu wa force account.


AGENDA: BZ/2021/2022/15 KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao iliyopelekeza kikao kumalizika kwa ufanisi. Aidha alitaka Secretarieti kuhakikisha kuwa taratibu za ujenzi wa madarasa hayo zinaanza haraka iwezekanavyo kwa kuzingatia muongozo wa mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa Umma, sheria ya ununuzi na kanuni zake mwisho alifunga kikao saa 5:45 Asubuhi.

UMEDHIBITISHWA



HERIBET BILIA
MWENYEKITI



ZABDIEL MOSHI
KATIBU

TAREHE: 18/11/2021
